

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

MKUU WA MKOA WA NJOMBE

SIMU: 026- 2790001

FAX: 026- 2790001



OFISI YA MKUU WA WILAYA,

S.L.P 02,

LUDEWA.

**JULAI 08, 2022**

**TAARIFA KWA UMMA**

Mkuu wa Wilaya ya Ludewa Mheshimiwa Andrea Tsere leo Julai 08, 2022 ameongoza kikao cha Kamati ya Lishe cha robo ya nne kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo katika kikao hicho wameshiriki viongozi mbalimbali akiwemo Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Ndugu. Sunday Deogratias.

Katika kikao hicho zimewasilishwa taarifa mbalimbali zikiwemo taarifa za idara mbalimbali, Taarifa ya Idara ya Afya, Taarifa ya Elimu Sekondari, Taarifa ya Idara ya Elimu Msingi, Taarifa ya Idara ya Mifugo na Uvuvi, Taarifa ya Maendeleo ya Jamii na Taarifa ya Shirika la IMA World Health, akiwasilisha taarifa hiyo Afisa Ufuatiliaji wa Mradi wa shirika hilo Bi. Neema Lazaro.

Katika hatua nyingine Mhe. Andrea Tsere amewaagiza Maafisa Elimu Sekondari na Msingi kuhakikisha kila shule ya Wilaya ya Ludewa iwe na bustani ya mbogamboga na matunda pamoja na kuhakikisha wafugaji wote wanafugia ng'ombe wao kwenye mazizi na sio kuziacha porini.

**Chrispin B. Kalinga**  
**Afisa Habari na Mawasiliano Serikalini**  
**Halmashauri (W) Ludewa**

